**HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. JOSHUA MIRUMBE, MKUU WA WILAYA YA BUNDA KATIKA SHUGHULI YA UZINDUZI WA JUKWAA LA KILIMO – M-KILIMO, BUNDA 11/06/2014**

Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo zimekua zinatekeleza malengo ya milenia (MDGS). Nchi yetu ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa malengo hayo. Tathmini ya utekelezaji wa malengo ya millennia iliyofanyika mwaka 2008 iliguandua kuwa kasi ya ufikiaji wa malengo hayo ni mdogo na kunahitajika mikakati ya uharakishaji ya kuyafikia malengo hayo.

Moja katika changamoto ambazo zilichelewesha ufikiaji wa malengo ya millennia ilikua ni kukosekana mbinu za utoaji taarifa kwa wananchi Wananchi wengi hasa wa vijijini hawakupata taarifa muhimu zinazohusu maendeleo yao, hususan taarifa za kilimo.

Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu. Zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wa Tanzania wanategeme kilimo na ni muhimu sana katika kupunguza umaskini. Tehama inachangia kwa kiasi kikubwa katika kufikisha taarifa kwa wananchi wengi kwa haraka na usahihi.

Takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya watanzania milioni 20 wanamiliki simu za mkononi, kulingana na utafiti uliofanywa na ESRF hapa Bunda mwaka jana (2013) zaidi ya 80% ya wananchi waliohojiwa wanamiliki simu za mikononi. Hata hivyo pamoja na ongezeko hilo kubwa swali kubwa ni jinsi gani simu za mkononi zinaweza kutumiwa kuboresha maisha ya wananchi na hatimaye kupunguza umasikini wa kipato.

Katika jitihada ya kutatua changamoto zilizotajwa hapo juu , ESRF kwa msaada wa Serikali ya Tanzania na UNDP wameanzisha jukwaa, yaani Mobile Kilimo litakalosaidia kuwapatia wananchi fursa ya kupata taarifa zinazohusu ushauri wa kilimo bora ili kuongeza uzalishaji na hatimaye kuinua kipato cha

wananchi. Kupitia jukwaa hili wakulima wataweza kubadilishana uzoefu na hivyo kuboresha kilimo katika maeneo yao. Uanzishaji wa JUKWAA hili utasaidia kwa kiwango kikubwa kuongeza kasi ya kuharakisha kufikia malengo ya Millenia na kuleta maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Wakulima kupitia jukwaa hili watapata taarifa kuhusu masoko ya mazao na hivyo kuamua wapi wakauze mazao yao kwa faida zaidi. Kupitia jukwaa hili biashara na utoaji taarifa vitafanyika wakati wowote na siku yoyote (24/7).

Kwa kutumia jukwaa hili wataalamu wa kilimo wataweza kutoa taarifa za kilimo ikiwa ni pamoja na taadhali kuhusu hali ya hewa, majanga ya asili n.k, alikadhalika taarifa kama; misimu ya kilimo, na ushauri mbalimbali wa kilimo vitatolewa. Jukwaa hili litawasaidia kupunguza ghalama na muda wa kusafiri masafa marefu kutafuta masoko ya mazao.

Wilaya ya Bunda itashirikiana na UNDP na ESRF kuona jukwaa hili linafikia malengo yake.

Nimefurahishwa sana uamuzi kwa kuchagua wilaya ya Bunda kuwa ya kwanza kutekeleza mpango huu (mobile kilimo) Nimatarajio yangu kwamba wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara watalitumia jukwaa hili kutangaza bidhaa zao za kilimo na kutafuta masoko kwa kutumia simu za mkononi.

Napenda kuwashukuru sana ESRF na UNDP kwa uamuzi wao wa kuandaa jukwaa hili.

Kwa haya machache ningependa kusema kuwa jukwaa hili "Mobile Kilimo" limezinduliwa rasmi.

**AKSANTENI.**